**WHAT DOES THE BIBLE SAY ABOUT GOING TO CHURCH?**
**BIBLIA INASEMA NINI KUHUSU KWENDA KANISANI?**

I. Biblia huonyesha kwamba shauku ya kusikiliza na kujifunza neno la Mungu ni alama ya Mkristo.

**-Yoh 8:47**. Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu, hivyo ninyi hamsikii kwa sababu ninyi si wa Mungu.

**-Yoh 8:31**. Basi Yesu akawambia wale wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.

**Mdo 17:11**. Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalovyo.

**Zab. 119:72**. Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu, kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.

I **Thes 2:13**. Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu na ndivyo ilivyo kweli kweli, litendalo kazi pia ndani yenu ninyi manaoamini.

**Zab 1:2.** Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo na sheria yake huitafakari machana na usiku.

**II. Biblia huonyesha haja hii hutafuta ukamilishaji wake katika ibada ya wazi katika kanisa**

**Zab. 122:1.** Nalifurahi waliponiambia na twende nyumbani mwa Bwana.

**Lk 24:53.** (Wanafunzi) Nao walikuwa daima ndani ya hekalu wakimsifu na kumbariki Mungu.

**Mdo 2:46.** (Wakristo) walidumu kushika fundisho la mitume, na ushirika katika kuumega mkate nyumba kwa nyumba na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa Moyo mweupe.

**Ebrania 10:25**. (Wala tusiache) Kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo kwa kadri mwonayo siku ile kuwa inakaribia.

**Zab 26:8**. Bwana nimependa makao ya nyumba yako na mahali pa maskani ya utukufu wako.

**Kol 3:16**. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote mkifundishana na kuonyana kwa Zaburi na nyimbo na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.

**Luka 4:30 -31**. Lakini yeye alipita katikati yao akaenda zake. Aka shuka mpaka kapernaumu mji wa Galilaya, akawa akiwafundisha siku ya sabato

**Hosea 4:6**
Kwa kuwa umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe.

**LK 14:17-24**
Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari, wakaanza wote kutia udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, nimenunua shamba sharti niende nikalitazame tafadhali unisamehe. Mwingine akasema nimenunua ngombe jozi tano ninakwenda kuwajaribu tafadhali unisamehe. Wingine………..

**Luka 4:16.** Akaenda Nazareti hakupokelewa na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake akasimama ili asome.

**Marko 14:49**. (Yesu alisema) Nalikuwa nanyi kila siku katika hekalu nikifundisha na hamkunikamata.

**Zab 95:2.** Tuje mbele zake kwa shukrani tumfanyie shangwe kwa zaburi.

**Zab 27:4.** Neno moja nimelitaka kwa Bwana, nalo ndilo nitakalolitafuta, Nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu….Kutafakari hekaluni mwake.

**Zab 84:2.** Nafasi yangu imezionea shauku nyua za Bwana, moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye hai.

**III. <u>Biblia huonyesha baraka ambazo hutokana na kulisikia na kujifunza neno laMungu.</u>**

**Zab 84:4.** Heri wakaao nyumbani mwako.

**Ipet 1:23.** (ONGOA/FUFUA) kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iharibikayo bali kwa ile isiyoharibika kwa neno la Mungu lenye uzima lidumulo hata milele.

**Yakobo 1:21** (WOKOVU)

- Kupokea kwa upole neno, ambalo liwezalo kuziokoa roho zenu.

**Mdo 11:14.** (Petro) Atakaye kuambia maneno ambayo yatakuakoa wewe na nyumba yako yote.

**Yohana 17:17** (UTAKASO)

- Uwatakase kwa ile kweli neno lako ndiyo kweli

**Wagalatia 3:2**. (ROHO MTAKATIFU)

- Nataka kujifunza neno hili moja kwenu mlipokea Roho kwa matendo ya sheria au kwa kusikia kunakotokana na imani?

**RUM 10:17** (IMANI)

- Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia haya kwa neno la Kristo.

**Yoh 10:27-28** (UZIMA WA MILELE)

-Kondoo wangu waisikia sauti yangu nami nawajua, nao wanifuata. Nami na wapa uzima wa milele, wala hawatapotea kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu.

**Yohana 5:24.** Amani Amani nawaambia, yeye aliyenipelekea yuna uzima wa milele, wala haingii hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.

**Yoh 5:39.** Mwayachunguza maandiko kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake, na hayo ndiyo yanayo nishuhudia.

**Yohana 8:31-32** (UKWELI NA UHURU)

Basi Yesu akawaambia…."Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. Na mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru.

**Mathayo 6:33** (VITU VYA KIMWILI)

Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake na hayo yote mtazidishiwa.

**UFUPISHO** (II TIMOTHEO 3:15-17)

Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa Imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza na kwa kuwadibisha katika haki. Ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.

**Biblia hu hadharisha wote ambao hawasikilizi Mahubiri na Neno la Mungu.**

**Yohana 8:47.** Yeye aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu hivyo ninyi hamsikii kwa sababu ninyi si wa Mungu.

**Zaburi 95:7-11**

Leo, kama utaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu…kwa miaka 40 nalihusunika na kizazi kile, nikasema hao ni watu waliopotoka mioyo. Hawakuzijua njia zangu. Nikaapa kwa hasira yangu wasiingie rahani Mwangu.

**Amosi 8:11**
Angalia siku zinakuja aseme Bwana Mungu ambazo nitaleta njaa katika nchi, si njaa ya kukosa chakula wala kiu au kukosa maji bali ya kukosa kuyasikia maneno ya Bwana.

**LK 10:16**
Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma.

**Mithali 13:13**
Kila alidharauye neno hujiletea uharibifu bali yeye aiogopaye amri atapewa thawabu.

Hili kwa wengi linaonekana ni kiburi na kuhukumu. Kama kanisa hili lilikuwa na aina moja ya umoja katika ukweli. Hatuhisi kwamba, sisi ni watu pekee katika dunia ambao watakuwa wameokolewa. Hatutangazi kuwa wenye hekima na watakatifu sana kuliko wengine. Zaidi tunatangaza kila anayejiangalia nafsi yake mwenyewe, kama Paulo, kuwa watenda dhambi wa kwanza. Hatujionyeshi kuwa twastahili ushiriki (meza ya Bwana). Licha ya hilo, hatustahili kuwa ndani na sisi wenyewe. Inatupasa kuamini kiuthabiti ingawa kwamba Biblia hushikilia jinsi ya kuwa, neno la Mungu lote katika sehemu zake. Tunaamini Biblia ni sahihi kwa kile inachokifundisha, na mafundisho yote yake ni muhimu. Hitimisho, tunaamini kwamba lazima kuwe na umoja wa uhakika kwa kuangalia neno la Mungu labla kama umoja katika Imani iliyoelezwa katika ushirika (meza ya Bwana). Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadabisha katika haki.

**<u>KUKAWIA SIO KUKATAA</u>**
Si kwa kualika wageni wetu (wa kiwango kingine cha ukiri) kujumuika nasi, tunachukua jambo la mashaka sana. Huhatarisha kuacha alama ambayo hujiendeleza yenyewe kwa kuwafanya kama binadamu siyo juu ya viwango vyetu. Siyo injili tuichukuayo. Tunashauku kushiriki sakramenti ya madhabahu na wale ambao tunashiriki Imani pamoja. Huomba kwamba punde wageni kuelewa sababu ya tendo letu kwamba watataka kuchunguza kwa usahihi zaidi kwa kuamini kwetu. Hivyo tunatoa maelezo na kutia moyo kwa kujianda kujumuika nasi kwa kuungama nasi katika ufahamu na umoja wa imani hivyo kuungama katika meza ya Bwana.

www.LutheranMissions.org